**University of Dar es Salaam**

**Library Repository** **https://libraryrepository.udsm.ac.tz**

Mwalimu J.K Nyerere Speeches and Statements

1985-07-29

# Hotuba ya Raisi Julius K. Nyerere katika Bunge

Nyerere, Julius Kambarage

Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali

Nyerere J. K (1985) Hotuba ya Raisi Julius K. Nyerere katika Bunge, Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Dar es salaam. p.39

http://41.86.178.5:8080/xmlui/handle/123456789/7256

*Downloaded from University of Dar es Salaam Library Repository*

EAFPAM
JQ3516
.T36
N9

# HOTUBA YA RAIS JULIUS K. NYERERE KATIKA BUNGE

*Dar es Salaam* *29 Julai, 1985*

*Bei Sh. 10/-*

# HOTUBA YA RAIS MWALIMU JULIUS K. NYERERE KATIKA BUNGE
## DAR ES SALAAM, JULAI 29 1985

Ndugu Spika; na Waheshimiwa Wabunge

Kwa kuwa hii ndiyo mara yangu ya mwisho kulihutubia Bunge hili, leo napenda tuyatazame baadhi ya mambo tuliyoyafanya tangu nilipokabidhiwa mara ya kwanza jukumu la kuiongoza nchi yetu huru. Napenda kuyatazama mambo hayo kulingana na shabaha tulizojiwekea mwaka 1961, 1962, na 1964. Kupitia kwenu, napenda kuwaeleza mambo hayo wananchi walionichagua mara kwa mara kuiongoza nchi hii. Na pia napenda kutoa maoni yangu ya awali kuhusu mafanikio na matatizo nitakayomkabidhi Rais mpya kuyakabili, akishirikiana na Bunge lijalo.

Kazi iliyokuwa muhimu kuliko zote, kwangu mimi, na kwa wananchi wote, niliyoiazimia katika hotuba yangu ya kwanza mwezi Desemba 1962, ilikuwa ni kazi ya kujenga taifa lenye umoja kwa msingi wa heshima na usawa wa binadamu. Nilipolihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka mmoja kabla ya hapo, nilitoa ahadi vile vile kwamba msingi wa vitendo vya taifa letu utakuwa kufanya jitihada ya dhati ya kudumisha heshima na usawa wa binadamu, nchini mwetu na pengine duniani. Na kauli hiyo hiyo ya umoja ndiyo iliyokuwa kiini cha maneno yangu nilipolihutubia Bunge Aprili 25, 1964 wakati nilipoliomba Bunge kuthibitisha makubaliano ya kuunganisha nchi mbili huru, Tanganyika na Zanzibar.

Nadhani naweza nikasema bila kusita kwamba mnamo chini ya miaka 25, kwa shabaha hii kuu na ya msingi kupita zote, tunayo haki ya kujivuna. Sasa tunalo Taifa, na taifa lenye umoja. Tunalo taifa ambalo msingi wake ni heshima na usawa wa binadamu. Na tumepiga hatua kubwa sana katika kuuimarisha umoja huo.

Jambo moja la msingi katika kujenga na

DB

kulinda umoja wa taifa letu ni kwamba kwa Katiba ya taifa letu na Katiba ya Chama chetu, na vile vile kwa mazoea na msimamo imara wa muda mrefu, nchi yetu haina dini yake. Wananchi wana dini zao, ambazo wana uhuru kamili wa kuzifuata na ambazo zinaheshimiwa kabisa, mradi wasivunje sheria zetu. Lakini nchi yenyewe haina dini yake rasmi; na Chama chenyewe hakina dini yake rasmi. Viongozi wetu huchaguliwa, na kuendelea kushika madaraka yao, bila ya kujali imani zao au dini zao. Huchaguliwa kwa sababu ya sifa zao wenyewe, au vitendo vyao, na jinsi wanavyojitolea kuwahudumia watu wetu na taifa letu. Kama wanakwenda Kanisani, au Msikitini, au Hekaluni; au kama hawaendi ko kote, si jambo la kuzingatiwa. Na lazima liendelee kuwa jambo ambalo halina uhusiano wo wote na kuchaguliwa kwao, au na vitendo vyao baada ya kuchaguliwa.

Jambo hili ni la msingi sana. Nusu ya wananchi wa nchi hii ni vijana ambao hawafahamu, na wengine wengi ni watu wazima ambao wamesahau, kwamba kabla hatujapata uhuru wetu tulikuwa watu tuliogawanywa kwa tabaka za rangi na za dini. Taifa letu jipya lilirithi ubaguzi wa rangi na wa dini uliokuwa umejengeka kwa sheria na kwa mazoea. Huduma za elimu na za afya zilikuwa zimegawanywa kwa kufuata rangi; uwakilishi katika Bunge ulifuata rangi; hata sehemu za kuishi zilikuwa zimetengwa kwa kufuata rangi za watu, na kadhalika. Nafasi za kazi zilikuwa zikitolewa kwa kufuata rangi; shule za serikali zilikuwa chache, na shule za madhehabu ya dini zilikusudiwa kwa wafuasi wa dini hizo.

Ubaguzi wote huo ulitoweka haraka sana baada ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali zetu daima zimepinga vitendo vyo vyote vya ubaguzi kwa misingi ya rangi, dini au ukabila. Na Tamko la Haki za Binadamu lililoingizwa katika Katiba zetu mpya linakataza,

kwa mujibu wa sheria, vitendo vyo vyote vya ubaguzi wa rangi au kabila, au dini vinavyoweza kutokea kwa sababu ya mabaki ya tabia za ubaguzi wa rangi au wa dini tuliorithi. Sisi sasa ni taifa la raia walio sawa kabisa mbele ya sheria: kwa nadharia na kwa vitendo.

Kazi itakayochukua muda mrefu zaidi, na kwa njia nyingine itakayokuwa ngumu zaidi, itakuwa ni ile ya kuzuia kuongezeka kwa tofauti mpya za mapato kati ya raia wa nchi hii, na kupunguza tofauti zile tulizozirithi. Lengo letu limekuwa kujenga Ujamaa. Tumepambana na unyonyaji wa mtu kumnyonya mtu kwa kutaifisha njia kuu za uchumi, na kujitahidi kutoa nafasi sawa za huduma za umma kwa kutumia taratibu za kodi na sera ya mapato, na kwa kutumia taratibu za mipango ya uchumi.

Tumepata mafanikio makubwa. Ushahidi wa mafanikio hayo ni kwamba uwiano wa mapato ya watu wa mijini, baada ya kutozwa kodi, umepungua kutoka makadirio ya 18.8:1 mwaka 1962, mpaka 15.7:1 mwaka 1966, kufikia 4.9:1 mwaka jana. Maana yake ni kuwa: katika mwaka 1962 pato la juu lilikuwa ni karibu mara 19 ya pato la chini; mwaka jana pato la juu lilikuwa ni karibu mara tano ya pato la chini. Hii ni hatua kubwa sana. Lakini haya ni mapambano yasiyokuwa na mwisho; juhudi zetu lazima ziendelee. Maana baadhi ya mila na taratibu zetu za urithi nchini mwetu zinamwezesha mtu mmoja kulimbikiza sana mali; ingawa baadhi hugawanya zaidi mali ya urithi. Na wezi, walanguzi na wafanya magendo mara nyingi sana hukwepa kodi na sheria nyingine zilizowekwa kuzuia vitendo vyao haramu. Vile vile unyonyaji unaweza kutokea kwa sababu ya watu kutumia vibaya wadhifa wao, au kwa sababu ya uzembe wa wale waliokabidhiwa kazi ya kuhudumia umma. Utaratibu upo wa kuondoa maovu hayo, lakini wakati mwingine utaratibu huo haufanyi kazi vizuri

sana.

Umoja wa nchi yetu vile vile umeimarishwa kwa hatua za makusudi na mafanikio ya kuendeleza zaidi lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa letu, na kwa kufufua makusudi utamaduni wetu. Naamini kwamba kama tukiendelea na juhudi zetu za sasa kuimarisha matumizi na mafunzo ya Kiswahili, lugha yetu na utamaduni wetu sasa hivi vimekomaa kiasi cha kutosha kutuwezesha kuanza upya kufundisha Kiswahili cha dunia, yaani Kiingereza.

Sisi sasa ni Taifa. Na kwa matakwa ya wananchi wenyewe wa sehemu zetu mbili, sisi ni Jamhuri ya Muungano. Taifa letu ni Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Ni taifa linalojivuna, na taifa ambalo limepata heshima katika mataifa kwa sababu ya siasa yake ya kutokufungamana na upande wo wote, kupinga ukoloni, na vile vile kwa sababu ya jitihada zake za ndani.

Sasa hivi uananchi wetu hautokani na mipaka tu ya nchi yetu, au bendera, au wimbo wa taifa, au mizinga 21 anayopigiwa Rais wake. Uananchi wetu umo ndani yetu wenyewe, wanachi wa Tanzania. Tunajua kwamba sisi ni Watanzania, na kwamba tunashiriki kwa ukamilifu katika kuiendesha nchi yetu: katika maendeleo yake, na katika kulinda heshima yake, kama ilivyodhihirika wakati Tanzania ilipovamiwa mwaka 1978. Wala uananchi wetu, au heshima na matarajio ya taifa letu, hayategemei tabia, uwezo, au ubovu wa mtu mmoja, awe Julius Nyerere, au Alli Hassan Mwinyi, au mwingine ye yote. Katika kipindi kifupi toka nchi zetu zipate uhuru, na toka kuanzishwa kwa Jamhuri yetu ya Muungano, tumejiundia taratibu na vyombo vinavyotuwezesha, kwa pamoja, kutawala na kuendesha nchi yetu. Rais wetu ni mtu muhimu; lakini yeye si Tanzania. Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar ni mtu muhimu; lakini yeye si Tanzania. Sisi, wananchi wote wa

Tanzania tuliounganika pamoja, ndio Tanzania.

Wakati wa uhuru, Serikali kilikuwa chombo cha kutawala na kulinda amani. Hakikuwa chombo cha maendeleo ya watu au uchumi wao; na hakikuwa chombo cha kidemokrasi. Sasa hivi hali ni tofauti kabisa. Serikali inaongoza na kusimamia maendeleo ya Tanzania, hiyo ndiyo shabaha yake ya kwanza; na sababu ya kutawala na kulinda amani ni kuimarisha shabaha hiyo. Kwa hiyo Serikali ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara zetu za Muungano, taratibu zetu za Baraza la Mawaziri (au Baraza la Mapinduzi), utawala wetu wa Mikoani, Idara zetu zinazotoa huduma, zimeundwa kwa shabaha hiyo hiyo. Vyombo hivi ni tofauti sana, na vimepanuka zaidi, kuliko vilivyokuwa mwaka 1961 au 1964.

Na kutoka muundo wa Kiingereza wa Serikali na Bunge la vyama vingi tuliouiga hapo mwanzo, tumejijengea utaratibu wa demokrasi ya Chama Kimoja unaolingana na hali ya Jamhuri yetu ya Muungano. Chama chetu, Chama cha Mapinduzi, kinaweka malengo, kinapanga umuhimu na misingi ya serikali na ya maendeleo. Serikali na Bunge hutafsiri misingi hiyo kwa sheria na katika utekelezaji, wakiwajibika moja kwa moja kwa umma kwa njia ya kura ya kila mtu mzima, na wakiwajibika vile vile kwa Chama kwa sababu ya uanachama wao na mashauriano ya mara kwa mara katika mambo makubwa.

Hatukuipata Katiba yetu ya sasa, au utaratibu wa utawala, kwa mara moja; wala hatusemi kwamba taratibu zetu za sasa hazitabadilika. Tumebadili Katiba ya Chama na Katiba za Serikali mara nyingi, ama kutokana na mahitaji mapya, ama kasoro zilipoonekana. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa miundo ya utawala au ya kazi za maendeleo. Wakati mwingine tumefanya makosa ambayo imetulazimu kuyasahihisha baadaye.

Tulianza uhuru wetu tukiwa na taratibu za utawala zilizoshikilia madaraka yote mahali pamoja, ili iwezekane kuwatumia kwa ukamilifu wasomi wachache waliokuwako wakati huo. Muundo huo ambao haukuwa imara na uliokuwa mbali na watu ulikuwa na hatari kwa uhuru, hasa kwa sababu ya kukosekana kwa vyombo ambavyo kazi yake ni kupinga na kukosoa Serikali. Kwa hiyo mwaka 1965 tuliunda Tume ya Kudumu ya Uchunguzi kuwazuia watu wenye madaraka wasiyatumie madaraka yao vibaya. Tume hii inaendelea kufanya kazi vizuri, ikipokea kiasi cha malalamiko ya maandishi 2,500 kwa mwaka. Mengi ya malalamiko hayo ama hayana msingi ama walalamikaji hawakutumia kwa ukamilifu njia zilizopo za kumaliza malalamiko yao; lakini wastani wa asilimia 15 ya malalamiko kila mwaka kusikilizwa na kuamuliwa. Kuanzia mwaka 1980 Tume hii inafanya kazi katika Jamhuri nzima ya Muungano.

Mwaka 1972, baada ya maendeleo ya kutosha ya kuwapa wananchi madaraka, tuligawa madaraka ya serikali katika ngazi za Mikoa na Wilaya, na wakati huo huo tukafuta utaratibu wa zamani wa Serikali za Mitaa. Mwaka 1975, kwa Sheria ya Vijiji, tuliweka misingi ya Serikali za Vijiji. Kufikia mwaka 1982 tukatambua kwamba tulifanya kosa kubwa kwa kufuta Serikali za mitaa; kwa hiyo Bunge likapitisha sheria ya kuunda tena Serikali za Mitaa wilayani na mijini, na kuacha taratibu zile nyingine ziendelee.

Lakini ingawa yametokea mabadiliko mengi, mwelekeo wa Katiba na wa utawala umebaki ule ule tokea uhuru. Tumekuwa tukijaribu kujiwekea taratibu za maendeleo ya kidemokrasi ya taifa letu, yanayowategemea wananchi wenyewe. Na pamoja na kasoro zake zote, ambazo lazima ziendelee kusahihishwa kila inapolazimu, naamini

kwamba taratibu zetu za serikali na za mipango ya maendeleo zimefanya kazi, na zinaendelea kufanya kazi, katika mwelekeo uliotarajiwa.

Mwelekeo wenyewe ulidhihirika zaidi kadiri tulivyoendelea kupata uzoefu. Maana ingawa mwaka 1963 tulikomesha taratibu za mtu kumiliki ardhi kama mali yake, na mwaka 1965 tukakomesha Nyarubanja, kufikia mwisho wa mwaka 1966 tuligundua kwamba tofauti za utajiri na hadhi kati ya wananchi, na pia tabia nyingine zilizokuwa zinaleta mgawanyiko, zilikuwa zinaanza kujitokeza. Ili kusahihisha hali hiyo Chama cha TANU katika Azimio la Arusha la mwaka 1967 kilitangaza maana ya Ujamaa na Kujitegemea katika Tanzania. Tokea wakati huo Azimio la Arusha limekuwa ndiyo dira yetu, kama lilivyofafanuliwa zaidi katika Mwongozo wa 1971 na wa 1981.

Mwezi Februari 1967 tulitaifisha vyombo vikuu vya fedha. Naamini kwamba hatua hizo zilituwezesha kupata maendeleo mazuri ya uchumi mpaka mwisho wa miaka ya 1970, na kutupa nguvu zilizotuwezesha kuhimili kipindi kigumu kilichofuata tokea wakati huo. Maana kwa kutumia vyombo hivyo vya umma tumeweza kujenga huduma za kusambaza fedha katika maeneo ya vijijini na katika sekta nyingine za uchumi nchini mwetu, na vile vile kutumia rasilmali ya fedha zetu zote kwa ajili ya maendeleo ya nchi badala ya kuacha rasilmali yetu kidogo tuliyokuwa nayo iwekezwe au ihamishiwe mahali pengine.

Kwa hiyo, kwa mfano, ingawa kufikia mwaka 1966 tulikuwa tumekwisha kuchukua hatua ya kuanzisha Benki Kuu ya Tanzania, na kutengeneza noti zetu wenyewe, kabla ya Azimio la Arusha tuliweza kueneza huduma za Benki ya Biashara katika miji michache tu. Mwaka 1967 Benki zote za Biashara zilizokuwako zilikuwa na matawi 64 tu. Sasa Benki ya Taifa ya Biashara ina matawi 381. Pamoja na

Benki ya Biashara, sasa tunazo Benki tatu za rasilmali: moja ya Ushirika na Maendeleo ya Vijijini, moja ya Maendeleo ya Viwanda, na moja ya Ujenzi wa Nyumba. Benki ya Posta nayo inaendelea, na Zanzibar ina benki yake yenyewe: Benki ya Watu wa Zanzibar. Zaidi ya hizo, tuna Shirika la Bima letu wenyewe, na Akiba ya Taifa ya Wafanyakazi inayohudumia mahitaji ya wananchi wenyewe, na wakati huo huo kuwezesha akiba zao kutumika kwa maendeleo yetu wote mpaka hapo wenyewe watakapozihitaji. Kwa kweli, kwa hali ya uwezo wetu, tunaweza kusema kuwa Tanzania ina idadi kamili ya vyombo vya fedha vyenye uwezo wa kutoa mikopo ya aina nyingi ya muda mfupi na muda mrefu, pamoja na kukusanya na kuhifadhi akiba za wananchi.

Mwaka 1967, au mara baada ya hapo, ama tumetaifisha ama tumechukua hisa katika makampuni ya uzalishaji na ya biashara yaliyokuwa na manufaa kwa uchumi yaliyokuwapo wakati huo. Kwa kufanya hivyo tulitaka kusisitiza kwamba shabaha ya shughuli za uchumi ni manufaa ya wananchi, siyo faida tu ya mabepari. Lakini maendeleo ya kweli ya taifa letu yalianza hasa baada ya vitendo hivyo. Kabla ya Azimio la Arusha ni rasilmali kidogo sana iliyokuwa imetumiwa katika kuleta maendeleo ya wananchi.

Kwa hiyo, katika miaka sita ya uhuru wa Tanzania Bara, tulikuwa tumejipatia uwezo wa kuanza vita tulivyokuwa tumevitangaza Desemba mwaka 1961: vita vya kuondoa umaskini wa watu wetu. Na mafanikio tuliyoyapata si haba. Kwa bei za mwaka 1966 (yaani ukiondoa hesabu za kupanda kwa bei) pato la kila mtu katika Tanzania mwaka 1964 lilikuwa shilingi 510.8 kwa mwaka; mwaka 1966 (mwaka ambao ulikuwa mzuri sana kwa mazao ya kilimo) lilikuwa shilingi 557.1. Baada ya miaka 11 ya siasa ya ujamaa, kipindi ambacho tulipatwa na ukame wa miaka miwili na

kupanda kwa bei ya mafuta kutoka dola 1.5 hadi dola 13 za Marekani kwa pipa, mwaka 1978 pato la kila mtu lilifikia shilingi 680.1 kwa mwaka. Na kutoka mwaka 1967 hadi mwaka 1978, idadi ya watu ilikuwa imeongezeka kutoka milioni 11.7 kufikia milioni 17. Kwa hiyo pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu, pato la kila mwananchi lilikuwa likiongezeka mwaka hata mwaka, ingawa tulikuwa katika mazingira magumu.

Lakini kuanzia mwaka 1977, uchumi wetu umekumbana na mfululizo wa maafa mengi makubwa, na wala hatujaweza bado kuondokana na madhara yake. Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kulitulazimu kubadili mipango yetu ya uchumi kwa gharama kubwa sana. Ili kusahihisha hali hiyo ilibidi tuongeze katika mipango yetu ya maendeleo matumizi ya haraka ya kiasi cha shilingi 2,000 milioni ili kupata vifaa muhimu. Mwaka 1978 nchi yetu ikavamiwa; makadirio ya gharama ya vita vilivyofuatia ni kiasi cha shilingi 4,000 milioni. Na, mwanzoni mwa mwaka 1979, bei ya mafuta ambayo lazima tuyaagize kwa ajili ya usafirishaji na nishati ilipanda tena: kutoka dola 13 kwa pipa kufikia dola 36 za Marekani kwa pipa mnamo mwaka 1982.

Wala huo haukuwa mwisho. Kuanzia mwaka 1979, kwa miaka mingi mfululizo, tulipata ukame, na kwa sababu hiyo uzalishaji wetu wa mazao ukapunguka sana; katika misimu mitatu toka 1980 hadi 1983, tulilazimika kununua kutoka nchi za nje tani 632,600 za mahindi (pamoja na mchele na ngano) ili kulisha watu wa mijini pamoja na wale wa vijijini ambako mazao hayakupatikana.

Pamoja na matatizo hayo maalum ya Tanzania, vurugu iliyoongezeka katika uchumi wa kimataifa imeikumba Tanzania kama ilivyozikumba nchi maskini zote nyingine. Tumelazimika kuyakabili matatizo ya kuanguka kwa uchumi na

kukosekana kwa kazi katika nchi zilizoendelea, mabadiliko makubwa ya thamani za sarafu, viwango vikubwa mno vya riba za mikopo ya benki, na tabia iliyoongezeka ya nchi tajiri kuhami masoko yao. Na uwiano wa biashara ya kimataifa, ambao tangu uhuru umekuwa ukiwaumiza wazalishaji wa mazao-asilia, ulikuwa mbaya zaidi wakati bei za mazao-asilia zilipoanguka sana mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Ukizingatia yote hayo, si jambo la kushangaza kwamba kipindi cha Bunge hili kimekuwa kipindi ambacho pato la Taifa la kila mtu limeanguka sana. Mwaka 1983 (bado kwa bei za mwaka 1966) pato lilikuwa shilingi 589.4, ambalo lilikuwa chini zaidi kuliko wakati wo wote tokea mwaka 1968. Kwa juhudi za ajabu kabisa za serikali yetu na wananchi wenyewe, kufikia mwaka jana tulianza kuzuia kudidimia zaidi; kwa kweli Waziri wa Uchumi na Mipango ya Maendeleo aliliambia Bunge hili kwamba katika mwaka 1984 kumekuwako ongezeko dogo la asilimia 2.5 katika uzalishaji. Kwa bahati mbaya wakati huo huo idadi ya watu nayo imeongezeka kwa asilimia 3.3; kwa hiyo pato la kila mtu limeendelea kuanguka.

Ndugu Spika. Sura hiyo hiyo inaweza kuonekana katika kila sehemu ya uchumi wetu: kwanza kusonga sana mbele katika mapambano yetu ya kuondoa umaskini, halafu, kurudi nyuma katika kipindi cha miaka sita iliyopita.

Wakati wa uhuru, katika Tanzania Bara yote, kulikuwako viwanda ama vinu 220 vilivyoajiri zaidi ya watu 10 na vilivyokuwa na rasilmali ya zaidi ya shilingi 200,000. Shughuli ambazo kwa kweli tungeweza kuziita "viwanda" tungeweza kuzihesabu katika vidole vya mkono mmoja: ukiacha viwanda vya kusindikia pamba na kiwanda kimoja cha sukari, kulikuwa na kiwanda cha sigara, cha makopo, cha viatu, cha dawa na cha bia! Tulinuia

kuibadili hali hiyo, na kuweka msingi wa viwanda vyetu wenyewe, na siyo utaratibu wa kuwa na viwanda katika mnyororo wa viwanda vya makampuni ya kimataifa.

Mafanikio kidogo yalikuwa yamepatikana kutokana na juhudi za Serikali na za Shirika la Maendeleo ya Taifa lililoanzishwa mwaka 1965. Lakini kufikia Februari 1967 bado zilikuwako shughuli saba tu za viwanda ambazo zilikuwa zina umuhimu wa kutosha katika maendeleo yetu hata kutufanya tuzitaifishe. Maendeleo hasa yalipatikana katika kipindi cha kati ya Azimio na miaka ya 1970, kwa juhudi za makusudi kabisa za kila Serikali iliyochaguliwa, na Mashirika ya Umma yaliyoundwa.

Sasa hivi siwezi tena kutoa orodha kamili ya viwanda vyetu: orodha hiyo ingekuwa ndefu mno. Sasa tunavyo viwanda vyenye uwezo wa kutengeneza karibu nguo zetu zote tunazozihitaji, kama tungeweza kutumia uwezo wake wote. Ukiacha viwanda vingi vinavyotengeneza bidhaa za matumizi ya kawaida, tunavyo viwanda vya viatu na vya bidhaa za ngozi, na viwanda vya kutengenezea vifaa vya ujenzi (kama saruji), vya elimu, na madawa. Vile vile tunavyo viwanda vitatu vya kutengenezea zana za kilimo; tumeanzisha viwanda vya chuma na vya vyombo vya ufundi, kiwanda cha kuyeyushia chuma kutokana na vyuma vikuu-kuu; tuna kiwanda cha mabati, na kiwanda cha karatasi. Na vile vile tunacho kiwanda cha kuchongea mitambo ya viwandani. Maana tokea 1975 tumekuwa tukifanya jitihada ya kukamilisha lengo la kuwa na viwanda vya msingi, lengo ambalo litatilia mkazo zaidi ujenzi wa viwanda vitakavyotufanya tujitegemee zaidi katika kujenga viwanda vingine na katika utengenezaji wa bidhaa. Na kwa msaada wa Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo, pamoja na jitihada za Wilaya, Vijiji na za watu binafsi, sasa tunavyo viwanda vidogo vidogo 1,230 vijijini, pamoja na

vingine vilivyoko mijini.

Kwa hiyo hata kufikia mwaka 1979 tulikuwa tumepiga hatua nzuri sana katika kupanua shughuli zetu za viwanda. Kwa bei za kudumu, uzalishaji wa viwanda uliongezeka kutoka shilingi 572 milioni mwaka 1967 kufikia shilingi 1,429 milioni mwaka 1978, ongezeko la karibu asilimia 150. Kwa bahati mbaya, tulipokuwa tukijenga sekta hii ya uchumi wetu, hatukuzingatia sana suala la kuchagua aina ya viwanda na utaalamu uliolingana na hali ya uchumi wetu, hatua ya maendeleo yetu, na matatizo yetu ya usafiri. Na hatukuweza, na wala hatujaweza, kujenga uwiano unaofaa kati ya viwanda mbali mbali, au kati ya viwanda na sekta nyingine za uchumi wetu. Wala hatukuzingatia umuhimu wa matumizi ya kutunza viwanda vyetu. Kwa hiyo matatizo ya fedha za kigeni yalipozidi, uzalishaji katika karibu viwanda vyetu vyote ulishuka sana. Sasa hivi vinaweza kuzalisha kiasi cha asilimia 30 tu ya uwezo wake, au wakati mwingine chini ya hapo, kwa sababu vinategemea kuagiza spea, au mali ghafi kutoka nchi za nje, na fedha za kigeni hazipo kuagizia vitu hivyo. Mwaka 1983 jumla ya uzalishaji kutoka viwandani (kwa bei za mwaka 1966) ulianguka kufikia shilingi 603 milioni, kiasi ambacho ni asilimia 5.4 tu zaidi ya kile cha mwaka 1967!

Kitu kingine muhimu katika maendeleo yo yote ya viwanda ni upatikanaji wa nishati, na Serikali imeipa umuhimu mkubwa sekta hii. Kwa kweli inafaa tuipongeze Wizara na Mashirika mengine yanayoshughulikia nishati kwa juhudi zao kubwa na, pamoja na matatizo yaliyopo, mafanikio makubwa ya maendeleo yetu katika suala hili.

Kiasi cha umeme uliotengenezwa na kuuzwa katika Tanzania kimeongezeka kwa asilimia 420 toka mwaka 1961, na kiasi cha uwezo uliojengwa kimeongezeka kwa

asilimia 577. Sehemu kubwa ya maongezeko hayo inatokana na mitambo inayosukumwa kwa maji iliyojengwa toka tupate uhuru. Zaidi ya hapo, tunaendeleza kwa haraka mpango wa kujenga njia kuu kwa ajili ya kusambazia umeme huo; na hatua hiyo itasaidia sana kuondoa matatizo ya viwanda katika miji iliyo mbali na bandari zetu. Maendeleo yote hayo kwa pamoja yametupunguzia tatizo tulilolipata kutokana na uhaba wa fedha za kigeni, uliotulazimu kupunguza kiasi cha mafuta tuliyonunua kutoka nchi za nje kutoka tani 815,000 mwaka 1972 kufikia tani 687,000 mwaka 1984: na hata hayo bado tuna matatizo ya kuyalipia.

Wakati huo huo tumeendelea kutafuta mafuta yetu wenyewe. Kati ya mwaka 1969 na mwaka 1984 Shirika la Maendeleo ya Petroli, likishirikiana na makampuni ya watu binafsi, na kwa msaada wa fedha kutoka katika nchi za nje, limechimba visima 23 vya majaribio. Tumegundua kiasi kikubwa cha gesi, lakini kwa bahati mbaya bado hatujagundua mafuta. Wastani wa gharama ya kuchimba kisima kimoja mpaka sasa ni dola za Marekani milioni 15.2! Wakati tunapoendelea kutafuta mafuta, tunaendelea vile vile kutafuta fedha za kuchimbia gesi ili kutengeneza mbolea ya aina ya ammonia na urea. Mpango wa shughuli hii umekamilika.

Usafirishaji na Mawasiliano ni mambo mengine muhimu katika kuweka misingi ya maendeleo. Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hali yetu ilikuwa mbaya sana katika sekta hiyo.

Tulikuwa na Reli ya Uhuru ya kilometa 1,860 mpaka Tunduma tuliyoijenga kwa kushirikiana na Zambia kwa msaada mkubwa sana wa wananchi wa China. Lakini katika reli zetu nyingine tulijikuta mwaka 1977 tuna vifaa vikuu-kuu, (kati ya injini 140, 94 zilikuwa za kuendeshwa kwa mvuke); tulikuwa na reli ambayo haikuwa tu ya zamani

sana, maana sehemu yake kubwa ilijengwa wakati wa utawala wa Kijarumani, lakini vile vile haikutunzwa vizuri; na hatukuwa na vyuo vya mafunzo au karakana za kutengenezea injini zilizoharibika.

Ndugu Spika. Mara kwa mara huwa nawaona wananchi wakijipanga mistari mirefu kungojea kununua tikiti stesheni ya Dar es Salaam, na wakati mwingine wanalala papo hapo ili kuwahi kesho; najua kwamba kuna ucheleweshaji katika usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli. Lakini bado nadhani pongezi zinastahili kutolewa kwa juhudi zilizofanywa tokea mwaka 1977, hasa tukitambua matatizo yaliyokuwako katika kipindi hicho. Idadi kubwa ya injini na mabehewa mapya ya abiria na ya mizigo yamenunuliwa; reli yenyewe inatandikwa upya; awamu ya pili ya Karakana ya Morogoro imekamilika, na Karakana ya Dar es Salaam imetengenezwa upya. Vile vile meli mpya zimenunuliwa kutoa huduma katika maziwa yetu, na gati la kuzitengenezea meli hizo zinapoharibika limejengwa katika Ziwa Victoria.

Ujenzi wa bandari ulifanyika wakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; magati manane mapya na Makao Makuu ya Bandari yalijengwa kati ya 1967 na 1977. Kwa bahati mbaya haikuwezekana kuendelea zaidi na mipango iliyokuwapo ya ujenzi kuanzia hapo; mkopo wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kazi hiyo haukutolewa mpaka mwaka 1984, baada ya kumalizika kwa mgogoro wa mgawanyo wa mali za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuliifanya Tanzania iwe karibu haina kabisa huduma ya ndege mwezi Februari 1977. Shirika la Ndege la Tanzania liliundwa miezi michache baadaye kwa kurithi ndege mbili za aina ya Fokker 27 ambazo ziliweza kutumika, na moja ya aina ya DC 9 ambayo ilibidi iuzwe. Baada ya ndege yao ya

aina ya "Twin Otter" kuanguka mwaka 1984, Shirika la Ndege la Tanzania sasa lina ndege kumi, na nane tu katika hizo zimo katika hali nzuri. Karakana ya matengenezo madogo-madogo imekamilika, lakini matengenezo makubwa, ambayo lazima yafanyike katika vipindi maalum, bado lazima yafanywe katika nchi za nje kwa gharama kubwa ya fedha za kigeni. Kwa sasa Shirika hili limeimarika, na litaendelea kupanunuliwa na kuendeshwa kisasa zaidi, kadiri uwezo wetu utakavyoturuhusu.

Huduma za Posta na Simu vile vile zimeongezeka sana, na vyombo vyake ni vya kisasa zaidi. Sasa hivi tunazo simu 44,000 nchini kulinganisha na simu 19,000 wakati wa uhuru; tuna Posta, kubwa na ndogo, 719 kulinganisha na 185 zilizokuwako. Baada ya kunyimwa nafasi ya kukitumia kituo cha Afrika Mashariki, tumejenga kituo chetu wenyewe cha kupokea na kupeleka simu kwa kutumia "satellite".

Msingi wa biashara ya taifa vile vile umewekwa tokea kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Makampuni yetu ya Biashara, ya Taifa na ya Mikoa, sasa hivi ndiyo yanayochukua sehemu kubwa ya biashara ya jumla, ya kuagiza kutoka nje na kuuza nje. Makampuni hayo yaliundwa ili kuzitia huduma hizi muhimu mikononi mwa wananchi. Kwa bahati mbaya kazi yao katika miaka michache iliyopita ilikuwa kugawanya kwa usawa upungufu uliokuwako. Ukiacha bidhaa zilizotokana na mikopo kutoka nchi za nje, ambayo lazima ilipwe, na misaada ya maendeleo kutoka kwa rafiki zetu, bidhaa zinazoweza kununuliwa ni zile tu zinazotengenezwa nchini au zilizonunuliwa kutokana na mauzo yetu katika nchi za nje; na, kama nilivyokwisha kusema, umekuwako upungufu mkubwa sana wa mapato kutoka katika viwanda na kilimo tokea mwaka 1978.

Mpaka mwisho wa miaka ya 1960 Tanzania

ilikuwa na ziada kidogo ya fedha za kigeni katika nchi za nje: tuliuza mazao yenye thamani kubwa zaidi kuliko bidhaa tulizoziagiza. Hii inaonyesha kuwa hatukuwa na shughuli nyingi za maendeleo; bado tulikuwa tunajiandaa kwa mapambano ya kuupiga vita umaskini. Lakini thamani ya mazao yetu tuliyouza katika nchi za nje iliendelea kupanda mpaka mwaka 1977; ilianguka mwaka 1978 na kupanda tena na kufikia kilele kipya mwaka 1981, kabla ya kuanza upungufu unaoendelea mpaka sasa. Kwa upande mwingine thamani ya bidhaa tunazoagiza kutoka nchi za nje iliendelea kupanda mpaka mwaka 1980, ingawa kiasi chenyewe cha bidhaa tulizoagiza tayari kilikuwa kinapungua sana. Kufikia mwaka 1984, mauzo yetu katika nchi za nje yaliweza kulipia kiasi cha asilimia 41 tu ya bidhaa tulizoziagiza, bidhaa ambazo, kama wote tunavyofahamu kutokana na shida zetu za kila siku, hazitoshi hata kidogo kuendeshea uchumi wetu kwa ufanisi.

Hakuna dalili kwamba hali ya biashara yetu ya kimataifa, yaani thamani ya mazao tunayoyauza nchi za nje kulinganisha na ile ya bidhaa muhimu tunazoagiza kutoka nchi za nje, inaanza kuwa nzuri kwa upande wetu. Dalili za sasa ni kwamba hali itaendelea kuwa mbaya zaidi kwetu. Kwa mfano, kati ya Machi mwaka huu na sasa, bei ya kahawa katika soko la dunia imeshuka kwa zaidi ya Shs 25,000 kwa tani moja; na bei ya pamba vile vile imeshuka sana. Huo ndio ukweli wa dunia ambamo tunalazimika kujaribu kufanya biashara; na ni ukweli vile vile unaoeleza upungufu wetu katika uzalishaji, upungufu wa bidhaa, na kupanda kwa bei katika maduka yetu. Upungufu wa fedha za kigeni unaathiri kila kitu. Hakuna namna ya kukwepa. Nilipokuwa nasikiliza hotuba za mipango ya serikali na majadiliano yanayofuata katika Kikao hiki cha Bunge, nimeshangazwa na dalili za kuendelea kutoelewa

ukweli huu.

Hakuna mtu mwingine atakayetutatulia tatizo hili. Lazima tuongeze ufanisi katika uzalishaji na usambazaji wa bidhaa; lazima tulinde tulichokipata na kukitumia kwa yale mambo yaliyo muhimu kabisa, na lazima tuongeze mazao tunayoyauza katika nchi za nje. Lakini kwa vyo vyote vile lazima tuache kutamani bidhaa zinazotoka nchi za nje, na kugeuza mbinu zetu za uzalishaji zilingane na uwezo wetu na rasilmali zetu wenyewe. Na lazima tufanye hivyo haraka, na katika kila kitu.

Mbinu hii inahusu kilimo na uzalishaji mwingine wo wote. Matumizi mazuri ya ardhi yetu katika uzalishaji ndio msingi wa mafanikio yetu ya siku za baadaye. Na katika suala hili ufanisi wetu umekuwa mdogo mno. Wakulima wetu wanafanya kazi kwa bidii sana. Lakini baada ya karibu miaka 24 tangu nilipohutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza nikiwa Rais nikisisitiza umuhimu wa kutumia zana za kisasa za plau na trekta katika kilimo, inakadiriwa kwamba asilimia 79 ya kilimo chetu bado inaendeshwa kwa jembe la mkono. Aidha mbolea kidogo sana inatumika; na, lililo baya zaidi, matumizi ya mboji, samadi, na hata taratibu za asili za kupumzisha mashamba, zimepungua. Na misitu yetu inakatwa kwa wingi zaidi kuliko kiasi cha miti mipya inayopandwa. Kwa hiyo haishangazi kuona kwamba ongezeko la mazao yetu ya kilimo halilingani na ongezeko la watu, na kwamba rutuba ya ardhi yetu inapungua.

Haya hayakutokea kwa sababu ya kukosa siasa safi, lakini kwa sababu ya kushindwa kutekeleza siasa yetu. Agizo la Ujamaa Vijijini na Siasa ni Kilimo lilifuatiwa na Mikutano Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa juu ya Umwagiliaji Maji. Maazimio yote hayo yalitaka

matumizi ya mbinu na taratibu za kisasa, na kutilia mkazo zana zisizokuwa ghali sana na matumizi ya ujuzi na uzoefu uliokuwako katika sehemu fulani za nchi yetu. Na tumetambua wakati wote kwamba sehemu kubwa sana ya mazao ya chakula na ya biashara inategemea jasho la wakulima vijijini. Lakini badala ya kuwasaidia kutumia maarifa hayo na mengineyo, sisi tumewahutubia; tumeshindwa kuwapatia ama utaalamu ama hizo zana rahisi wanazozihitaji, na tukatumia rasilmali kidogo sana katika kilimo.

Si kweli kwamba tulirithi sekta nzuri sana ya kilimo wakati wa uhuru. Tanzania ililazimika kuagiza chakula kutoka katika nchi za nje kila mara katika miaka ya upungufu. Mwaka 1962 tuliagiza tani 69,000 za mahindi. Lakini ingawa uzalishaji wa chakula umeongezeka sana, idadi ya watu wetu imeongezeka kwa haraka zaidi. Sasa tunalazimika kuagiza chakula kutoka katika nchi za nje kila mwaka: hata mwaka huu, ambao unaonekana kuwa mwaka mzuri kuliko mwingine wo wote tokea 1978, yawezekana tusipate chakula cha kutosha kulisha watu wetu wote wanaoishi katika miji yetu. Na kiasi cha mazao yetu ya biashara kimeanguka sana.

Kwa mfano, mauzo ya pamba yaliongezeka kutoka tani 114,000 mwaka 1962/3 kufikia karibu tani 232,000 mwaka 1966/7; mwaka 1982/3 tuliuza tani 130,423 tu. Kutokea wakati huo mazao yamekuwa yakiongezeka tena kufikia tani 151,800 katika msimu uliopita. Msimu huu tunatazamia kuwa kiasi hicho kitashuka tena. Uzalishaji wa tumbaku ulipanda kwa haraka sana mpaka mwaka 1976/77; lakini sasa umeanguka kufikia uzalishaji wa mwaka 1970. Uamuzi wa makusudi ulifanywa katika miaka ya 1960 kupunguza uzalishaji wa mkonge, kwa sababu ya kuanguka sana kwa bei ya mkonge duniani; lakini haikuwa nia yetu

kupunguza uzalishaji kwa kiasi kikubwa namna hiyo kutoka tani 218,000 mwaka 1963 kufikia kiasi cha sasa cha tani 40,000. Ningeweza kuendelea. Korosho vile vile ni zao lingine lililoanguka; na karafuu kadhalika. Ni zao la kahawa peke yake, pengine na chai, lililoweza kuendelea kuongezeka pole pole. Wakati mmoja ilikadiriwa kwamba, hata pamoja na kuanguka kwa bei, tungeweza kupata shilingi bilioni moja zaidi ya fedha za kigeni kama tungeweza kuzalisha kiasi kile kile kikubwa cha mazao yetu makubwa.

Tukizitazama tarakimu hizo tena tunaweza tukapata funzo kubwa juu ya wapi tulipokosea. Katika karibu mazao yetu yote, na hasa katika mazao ya pamba, korosho, tumbaku na pareto, kulikuwako kipindi cha ongezeko kabla ya kuanza kuanguka. Katika mazao yote hayo, sababu kubwa ya ongezeko ilikuwa ni kupanuliwa kwa mashamba, matumizi ya mbegu bora, utunzaji wa mashamba, na hasa matumizi ya mbolea. Upungufu tuliouona tokea hapo hautokani wakati wote na kupungua kwa ukubwa wa mashamba yanamolimwa mazao hayo: mashamba yalimolimwa pamba na tumbaku hayakupungua sana. Mara nyingi sana upungufu umetokea kwa sababu rutuba imepungua katika ardhi, au uharibifu wa wadudu umezidi, au uangalizi wa mashamba umepungua. Lazima tuchunguze sababu za mambo hayo kutokea; maana kama tatizo lingekuwa zana tu ambazo wakulima wetu wanazitumia, basi baada ya kufikia kilele tungebakia katika kiwango hicho hicho, kusingetokea upungufu.

Maana yake ni kwamba hata pamoja na matumizi ya jembe la mkono, bado ingewezekana kuongeza sana uzalishaji kama tungetumia mbegu bora, kama tungepanda vizuri, kama tungeongeza rutuba ardhini ama kwa kutumia mbolea ama kwa njia za asili, na kulinda mazao yasiliwe na wadudu mashambani na katika maghala.

Katika Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM wa mwaka 1982 nilizungumza kwa kirefu sana juu ya matatizo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, na haja ya kuiweka sekta hii katika kiini cha mipango yetu yote ya uchumi. Mabadiliko hayo yameanza. Sasa sekta ya kilimo inapata sehemu kubwa zaidi ya fedha za maendeleo; Vyama vya Ushirika vimeanzishwa tena, kufutwa kwa vyama hivyo lilikuwa kosa lingine kubwa tulilolifanya katika miaka iliyopita; na shughuli za Wizara nyingine, pamoja na zile za mikoa na Wilaya, zinaelekezwa zaidi katika kukidhi mahitaji ya wakulima.

Maana lazima tukumbuke kuwa uzalishaji katika kilimo na mapato yake hayategemei shughuli zinazoitwa "za kilimo" au "maliasili" peke yake. Wakulima wanahitaji zana za kilimo, na wanahitaji bidhaa watakazozinunua kutokana na mapato yao: hizo ni shughuli za viwanda. Wanahitaji usafiri wa kuaminika kwa ajili ya mazao yao, na nishati ya kuwapunguzia jasho lao. Wanahitaji huduma za elimu na afya, na kadhalika. Vile vile wanahitaji heshima ya kuendesha shughuli zao wenyewe kijijini, na kushiriki katika serikali ya Wilaya yao na Taifa lao. Haiwezekani kutimiza kwa ukamilifu mahitaji ya wakulima kwa kupuuza mambo hayo yote mengine ya maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii katika Tanzania. Wala haiwezekani kutoa bei kwa mazao yao ambazo zinazidi bei zinazotolewa katika masoko ya dunia. Jumla ya wakulima ni kiasi cha asilimia 80 ya watu wote katika nchi yetu; hawawezi wao peke yao wakapata maendeleo wakati taifa zima limo katika matatizo ya uchumi kwa sababu ambazo hatuna uwezo nazo, na wala taifa haliwezi likapata maendeleo kama litapuuza mahitaji ya wakulima. Wao ndio sehemu kubwa ya taifa letu.

Na kwa upande wa wakulima hali yao si mbaya

sana. Tumepata mafanikio makubwa katika kutekeleza sera zetu za maendeleo ya vijijini na katika sera za kodi. Zamani watoto wa vijijini ndio waliokuwa hawana nafasi ya kwenda shule, sasa wanakwenda shule; watoto wa vijijini ndio waliokosa matibabu, na sasa wanayapata. Pato halisi la mkulima wa kawaida sasa ni kubwa zaidi kuliko la mfanyakazi wa mjini anayepata mshahara wa kima cha chini; katika maeneo ambako kuna zao zuri la biashara, mkulima aliyefanikiwa anaweza kupata pato kubwa zaidi kuliko watumishi wengi wa serikali, na wala hatalipa kodi kwa kiasi kile kile! Leo mkulima wa mahindi akiweza kupata hata magunia 50 tu katika shamba la hekta moja, atapata zaidi ya Shs. 24,000. Hata baada ya kuondoa gharama zake zote ni dhahiri kuwa pato lake linalobaki linazidi la mfanyakazi wa kima cha chini, ambalo ni Shs 9,600 tu kwa mwaka. Na mkulima ana hakika ya chakula chake na nyumba ya kulala, kwa sababu mara nyingi anajitegemea katika mambo hayo.

Lakini ukweli unabaki palepale kwamba kilimo chetu lazima kigeuzwe, kifanywe cha kisasa. Hatutaweza kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara kwa wakati mmoja mpaka tumeondokana na kutegemea jembe la mkono. Na jibu la mkulima, katika miaka michache ijayo, siyo trekta. Uwezo wa mkulima utaongezwa sana, na jasho lake litapunguzwa sana ikiwa tutaongeza matumizi ya plau na mikokoteni kwa kilimo, kwa usafirishaji wa vijijini, na zana nyepesi za kupukuchulia nafaka na kusaga unga. Ni wajibu wa uongozi kuhakikisha kwamba zana kama hizo zinapatikana kwa urahisi, na kwamba wakulima wanaelekezwa jinsi ya kuzitumia na kuzitunza. Na mazao ya mashamba yetu yataongezeka sana kama tutaongeza matumizi ya mbolea, samadi, mboji, pamoja na mikunde, kama marejea; na vile vile kwa kupanda kwa nafasi zinazotakiwa, kupanda mazao

yanayotakiwa, pamoja na njia nyingine za asili za kupambana na wadudu. Mambo haya si magumu kufanywa; basi natuyafanye. Maana tukiyafanya yataleta mabadiliko makubwa sana katika kilimo chetu na mapato ya wakulima wetu.

Ni jambo muhimu vile vile kwamba, kwa pamoja, tunatilia mkazo zaidi jambo la kupanda miti. Hata katika jambo hili kazi nzuri imekwisha kufanywa. Ukiacha upandaji miti unaohusiana na kiwanda cha karatasi cha Mufindi (ambao wenyeji wa pale wanasema kuwa umeongeza kiasi cha mvua inayonyesha katika sehemu ile), sasa hivi tunazo hekta 95,570 za misitu ya taifa, kulinganisha na hekta 3,340 tulizokuwa nazo wakati wa uhuru. Na upandaji miti katika vijiji umekuwa ukiongezeka kwa kiasi cha hekta 7,500 kila mwaka toka mwaka 1975. Hii ni juhudi kubwa, na pana haja ya kuiongeza. Pamoja na kusaidia kuzuia mmomonyoko wa ardhi, upandaji wa miti unahakikisha kupatikana kwa kuni na miti ya kujengea katika siku za mbele; ungeweza pia kuongeza mapato ya wanakijiji kwa kupanda miti katika ardhi ambayo haifai kwa mazao mengine.

Ndugu Spika na Waheshimiwa Wabunge. Pamoja na matatizo tuliyoyapata katika miaka michache iliyopita, naamini kwamba hayo niliyoyaeleza yanadhihirisha kwamba tumejiwekea misingi muhimu kwa ajili ya maendeleo ya uchumi, na kwamba hayo tuliyofanikiwa katika sekta hii vile vile yanatupa sababu ya haki ya kujivuna. Tumekuwa tukiendeleza mapambano ya kweli katika vita dhidi ya umaskini.

Lakini sifa kubwa ya Tanzania inatokana na mafanikio yetu katika kutoa huduma za umma. Hata maadui wa siasa yetu, baada ya kututukana na kutukashifu sana hulazimishwa na ukweli wakiri kwamba katika kutoa huduma

za umma nchi yetu imepiga hatua kubwa. Tuliamua kupambana na maafa ya ujinga na maradhi kwa sababu hiyo ni sehemu ya jitihada zetu za kujenga usawa wa binadamu, na kwa hiyo ni sehemu ya shughuli zetu za kujenga taifa; maana mapato ya kweli ya raia si fedha anazotia mfukoni mwake peke yake bali ni pamoja na kupata huduma za msingi za afya, elimu na nyinginezo. Na wakati huo huo kutumia fedha kwa ajili ya huduma za afya na elimu ni namna moja ya kuwekeza rasilmali ya kudumu katika amali ya taifa yenye thamani kuliko zote: yaani watu wake. Maendeleo ya kweli ya uchumi hayawezekani ikiwa wananchi ni wajinga, au wamelemewa na maradhi ambayo wangeweza kuyazuia.

Mwaka 1961 watoto wote waliokuwa katika shule za msingi walikuwa 486,000. Sasa hivi shule za msingi zina watoto 3,660,000. Hesabu hizo zinajieleza zenyewe. Ni mafanikio makubwa sana ya nchi yetu, mafanikio ambayo ni ya juu sana katika Afrika.

Zaidi ya hapo, elimu inayotolewa katika shule hizi hivi sasa inalingana zaidi na mahitaji ya Tanzania kuliko ilivyokuwa wakati wa uhuru. Watoto wote sasa wanakwenda shule kwa kipindi cha miaka saba Tanzania Bara, na miaka kumi na mmoja Tanzania Visiwani. Kabla ya Uhuru ni watoto wachache tu waliopata elimu ya msingi, na ambayo ilikuwa ya miaka minne tu. Vile vile masomo sasa yamebadilishwa kuwafanya watoto wajifunze mambo ya Tanzania na ya Afrika. Watoto wetu wanajifunza historia ya nchi hii, siyo ya Uingereza; wanajifunza Katiba yetu, na siyo nadharia ya Serikali ya watawala wetu. Wanajifunza Jiografia ya Afrika na ya Tanzania, na mambo ya msingi ya sayansi kutokana na eneo linalowazunguka. Sera ya Elimu ya Kujitegemea inatumika.

Ndugu Spika. Napenda kuchukua nafasi hii mara nyingine tena kutoa pongezi zangu na za Serikali kwa

walimu wetu, na hasa walimu wa shule za msingi. Wao wanalitumikia taifa zima, mara nyingi katika mazingira magumu sana. Tunawategemea sana. Mimi hufadhaika sana ninapogundua kwamba Kijiji, au Wilaya, au Wizara ya Elimu (kwa upande wa shule za sekondari) haijengi nyumba nzuri kwa walimu wake wote. Vile vile huwa na wasiwasi kama kweli wote tunaelewa maana ya kitu "elimu", nikiona wananchi vijijini, pamoja na wanachama wa CCM, wanachanga fedha kwa ajili ya shule ya sekondari, na kuacha shule zao za msingi bila madeski au viti au vifaa vingine muhimu vya kufundishia. Tunawadanganya watoto wetu tunapowapeleka katika shule za sekondari bila ya kuwawekea msingi mzuri katika ngazi hii muhimu ya awali, au bila ya kuwapa walimu mahitaji yao ya ubinadamu na vifaa vyao vya kufanyia kazi. Elimu ya msingi lazima iwe elimu bora kabisa, kwa sababu hiyo ndiyo elimu ya Watanzania wote.

Na kila tunapopata uwezo wa kupanua nafasi za elimu, lazima tutilie mkazo elimu ya ufundi, yaani maarifa ya kufanyia kazi: katika shule za msingi na kadhalika katika mafunzo ya baada ya hapo. Hiyo ndiyo sera ya serikali, lakini hiyo ni kazi moja ambayo hatujafanikiwa sana kuifanya. Watoto 6,700 tu kwa mwaka hupata nafasi katika vyuo vya ufundi; na vingi kati ya vyuo 316 tunavyovijua vimeandikishwa katika daftari tu, kwa sababu ama havina vifaa ama havina walimu; na wakati mwingine havina vifaa wala walimu. Serikali na Mashirika ya Kujitolea huendesha vyuo vya ufundi. Wizara ya Maendeleo ya Watumishi sasa inao wanafunzi 1,500 wanaojifunza kazi 36 mbali mbali katika vyuo vyao wenyewe, na wanafunzi wengine 4,700 wamehitimu katika kazi mbali mbali kutokana na mafunzo ya jioni. Yote haya ni mambo mapya; na vile vile utaratibu wa kutoa mitihani ya ufundi ni utaratibu mpya, ambao hao wanaohitimu katika vyuo vya

Mashirika ya Kujitolea na katika madarasa ya jioni wanaweza kuutumia. Mwaka 1966 watu 60 walijaribu mitihani hiyo; lakini mwaka 1983 watu waliofanya mitihani hiyo walikuwa 26,000.

Natumaini kwamba Bunge lijalo litafanya juhudi kubwa zaidi kusukuma elimu ya ufundi na elimu ya kazi kwa upande wa huduma yetu ya elimu, ingawa tunapaswa kutambua kwamba kipingamizi kikubwa ni kwamba vifaa vyote muhimu lazima viagizwe kutoka nchi za nje. Pia nimeyaomba Mashirika ya Kujitolea kutoa msaada mkubwa zaidi katika mpango huu; nimewahakikishia kwamba shule watakazozianzisha hazitataifishwa tena, kwa sababu hawatafanya dini kuwa ndiyo cheti cha kuingilia katika shule hizo, kama ilivyokuwa huko nyuma.

Kutilia kwangu mkazo Elimu ya Msingi maana yake siyo kwamba Serikali haikujishughulisha na elimu ya ziada. Hata kidogo! Miaka ya kwanza baada ya kujitawala tulitilia mkazo elimu ya Sekondari. Tulifanya hivyo makusudi, kwa sababu bila kufanya hivyo tusingeweza kupata walimu wa kutuwezesha kupanua elimu ya msingi. Mwaka 1961 wanafunzi katika shule za sekondari za serikali walikuwa 11,832; mwaka 1984 walikuwa 40,617, ongezeko ambalo ni maradufu kulinganisha na ongezeko la watu. Zaidi ya hayo, mwaka 1961 wanafunzi 236 tu kati ya hao walikuwa Kidato cha 5, ambapo mwaka 1984 vijana walioingia katika darasa hilo walikuwa 2,125. Vile vile limekuwako ongezeko kubwa la uwiano kwa wanafunzi wanawake katika shule za sekondari na katika Chuo Kikuu. Sasa hivi wanawake ni thuluthi nzima ya wanafunzi wote walio katika shule za sekondari, na asilimia 20 ya wanafunzi wote wa Chuo Kikuu.

Na kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanavyokumbuka, wakati wa Uhuru tulikuwa na Chuo kimoja

tu, wala siyo Chuo Kikuu, kilichokuwa kilichoanzishwa na Serikali ya Madaraka ya TANU. Chuo hicho kilianza na wanafunzi 14. Sasa hivi tunavyo Vyuo Vikuu kamili viwili vyenye wanafunzi wapatao 3,400. Kwa kiasi kikubwa sasa hivi tunajitegemea kwa upande wa kufundisha wanafunzi wa shahada ya kwanza; na kwa kweli katika masomo mengine ya sayansi tunazo nafasi bado ambazo hazijajazwa, kwa sababu mafunzo katika shule za msingi na za sekondari hayafikii kiwango cha kupata wanafunzi wa kutosha wanaoweza kumudu masomo ya Chuo Kikuu. Kiwango cha lugha ya Kiingereza kinachofikiwa vile vile ni kikwazo kikubwa kwa masomo katika Chuo Kikuu.

Maelezo haya hayajakamilisha mafanikio yetu katika maendeleo ya elimu. Mpango wa Elimu ya Watu Wazima, kwa madarasa, radio, magazeti ya vijijini, maktaba na masomo kwa njia ya posta umetutoa mahali ambapo asilimia 80 ya watu wazima walikuwa hawajui kusoma au kuandika, na kutufikisha mahali ambapo asilimia 85 ya watu wetu sasa hivi wanajua kusoma na kuandika. Katika jambo hili Tanzania inaongoza katika Afrika nzima; watu wetu wamekombolewa katika suala hili muhimu. Na mwaka jana karibu watu milioni 1.2 walihudhuria masomo yaliyopangwa na Wizara ya Elimu, baada ya kujua kusoma na kuandika!

Ningeweza kuelezea zaidi jambo hili Ukiacha Vyuo vya Elimu ya Taifa vinavyoendeshwa na Wizara ya Elimu, kila Wizara, na kila Shirika la Umma, lina mipango ya mafunzo kwa wafanyakazi wake. Mashirika mengi yanaendesha Vyuo vyao yenyewe. Kwa upande mmoja Jeshi la Kujenga Taifa ni chuo cha mafunzo; Jeshi la Wananchi lenyewe lina shule za sekondari na pia linatoa mafunzo ya ufundi; viko vile vile vyuo vingine: Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chuo cha Polisi, Vyuo vya Wizara ya Kilimo, Chuo cha Biashara, na kadhalika. Na kuna semina zisizokuwa na

idadi! Yote hayo ni sehemu ya juhudi ya kuinua uwezo wetu na ufanisi katika utekelezaji wetu. Mtu aliyesema kuwa Mapinduzi ya Tanzania ni Mapinduzi kwa Njia ya Elimu alisema kweli kabisa. Bado tuna kazi kubwa ya kufanya, lakini katika suala la elimu, sisi sasa ni watu tofauti kabisa na vile tulivyokuwa kabla ya uhuru.

Ndugu Spika na Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuwa zaidi ya nusu ya wananchi wa Tanzania wamezaliwa baada ya uhuru, watu wengi sana hawatambui ukubwa wa maendeleo tuliyoyapata katika huduma za afya tangu tujitawale.

Jambo moja kubwa katika masuala ya afya njema ni maji safi. Mwaka 1961 kiasi cha asilimia 11 ya watu wetu milioni 10 (yaani kiasi cha watu milioni 1.1) walikuwa wakipata maji safi. Sasa hivi chini kidogo ya asilimia 50, au wananchi zaidi ya milioni 10, wana maji safi katika umbali usiozidi meta 400 kutoka nyumbani kwao. Mafanikio hayo hayatoshi; maana yake ni kwamba nusu ya wananchi hawana maji safi karibu yao. Lakini bado ni mafanikio makubwa; tunaweza kujivunia hayo tuliyoyafanya mpaka sasa.

Takwimu za huduma za afya yenyewe nazo vile vile zinaridhisha. Wakati wa uhuru tulikuwa na hospitali 98, sasa tunazo 149; tulikuwa na vituo vya afya vijijini 22, sasa tunavyo 239; tulikuwa na zahanati 975, sasa tunazo 2,644. Kati ya hizi, hospitali 67, Vituo vya Afya 2, na zahanati 386 zimejengwa na zinaendeshwa na Mashirika ya Kujitolea, yanayosaidiwa ruzuku ya kiasi cha shilingi 44 milioni kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Idadi ya Watanzania wanaofanya kazi katika sekta ya afya vile vile imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Tulianza na madaktari wa Kitanzania 12 tu kwa watu

wetu zaidi ya milioni 10: yaani daktari mmoja kwa watu zaidi ya 830,000! Sasa hivi tunao madaktari 782 wa Kitanzania waliohitimu katika kiwango cha kimataifa: daktari mmoja kwa watu wapatao 26,000. Baadhi ya madaktari hawa ni mabingwa; na tunapata huduma za madaktari wageni 283. Tulikuwa na madaktari wasaidizi 32; sasa tunao 436 waliofunzwa kwa kiwango cha juu zaidi. Aidha, sasa hivi tunao Matabibu na Waganga wa Vijijini 6,328, watu muhimu ambao, licha ya mambo mengine wanayoyafanya, ndio wanaoziendesha zahanati na kliniki zetu. Ukichanganya madaktari na maadaktari wasaidizi, tulianza na daktari mmoja kwa watu zaidi ya 227,000: leo tuna daktari mmoja kwa watu wapatao 16,400. Bado hatuna madaktari wa kutosha. Lakini hatua tulizopiga tangu tujitawale ni kubwa sana. Upande wa Mabwana-Afya tu ndio tulioshindwa kuupanua kwa haraka; lakini kwa kuwa hawa ni muhimu kwa sababu ya kukinga maradhi, mpango wa kuwafunza mabwana afya wa vijijini umekwisha anza hivi karibuni.

Huduma zetu za afya ndizo hasa zilizosababisha vipimo vikuu vya afya Tanzania vionekane vizuri. Wakati wa uhuru watoto 225 kati ya kila 1,000 waliozaliwa hai walikufa wangali wachanga. Hesabu ya sasa ni watoto 137 kati ya kila 1,000. Na matarajio ya kuishi, ambayo kwa wastani yalikuwa miaka 35 wakati tulipoanza, sasa hivi yanakadiriwa kuwa miaka 51. Bado watoto 137 kwa kila 1,000 ni wengi mno; na umri wa miaka 51 ni mdogo mno; lakini vikilinganishwa na tulikoanzia, mafanikio yetu si haba. Tumeweka msingi wa kuleta maendeleo makubwa zaidi.

Ndugu Spika. Nilitoa pongezi kwa walimu. Madaktari na wauguzi wetu pia wanastahili pongezi nyingi. Tunao madaktari na wauguzi wazuri sana wanaofanya kazi katika nchi hii. Wao pia wamekuwa

wanafanya kazi na wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu sana. Kazi zao pia zinaathiriwa na upungufu wa fedha za kigeni ambao unaathiri huduma zetu nyingine. Ni jambo la uchungu sana kwa daktari kuona magonjwa anateseka au anakufa kwa maradhi ambayo angeweza kuyatibu kama angekuwa na dawa au vifaa vinavyotakiwa. Wao wanajitahidi kwa kadiri ya uwezo wao; na nchi haina budi iendelea kuwasaidia kwa kadiri ya uwezo wake.

Lazima tukumbuke pia kwamba sababu kubwa sana ya vifo na magonjwa katika nchi hii ni malaria na vidudu vingine vinavyosababisha kuharisha; nyingi ya sababu hizo zinaambatana na utapia-mlo au maji machafu. Tunao utaratibu wa tiba unaowawezesha watu wenye magonjwa makubwa au yasiyo ya kawaida kupelekwa kwenye Hospitali za Rufaa. Lakini kanuni za mwanzo za afya ndio msingi wa afya bora katika Tanzania. Lazima tuzipe kanuni hizo, na hasa upande ule wa kuzuia maradhi, umuhimu mkubwa katika makisio yanayotengwa kwa ajili ya shughuli za afya.

Ndugu Spika. Tunazo huduma nyingine nyingi za umma ambazo hata hatutambui kuwa zipo. Huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa na serikali bado ni kidogo sana; na tunayashukuru sana Mashirika ya Kujitolea kwa kuendesha vituo vyetu vingi vya watoto yatima, shule zetu za watoto walemavu, na mipango mingine inayowapa misaada au kuwapunguzia shida watu ambao wanastahili kuhudumiwa. Lakini huduma kama hizo zimeanza, na zinatoa msaada mkubwa sana kwa wananchi wenye matatizo; na Serikali inatoa msaada wa fedha kwa kazi hizo za kujitolea.

Wafanyakazi wana hakika ya kulindwa na vifungu vya usalama kazini vilivyoandikwa ndani ya sheria, na haki yao ya kupata kiinua mgongo endapo wataachishwa kazi bila wao wenyewe kufanya makosa. Lakini masharti haya yanategemea sheria iliyopitishwa na Bunge letu la

kwanza baada ya uhuru. Haikuwapo kabla ya uhuru. Sheria hiyo vile vile ilianzisha Akiba ya Taifa ya Wafanyakazi ambayo inahakikisha kwamba wafanya kazi wote, walio katika utumishi wa umma na walio katika sekta ya watu binafsi, angalau wanapata fedha kidogo wakati wanapostaafu. Mpaka sasa Akiba hiyo ina wanachama milioni 1.5. Mahakama ya Kazi yalianzishwa mwaka 1967, na yanafanya kazi kubwa kulinda haki za wafanyakazi. Huduma nyingine nyingi za mipango ya watumishi zinagusa maisha yetu na uchumi wetu, lakini tunazitambua tu wakati zinaposhindwa kutimiza yote yale zinazotarajiwa kuyatenda!

Kuhusu huduma mbali mbali ambazo zinalinda nchi yetu, pamoja na usalama na amani, hayako mengi ninayopaswa kuyasema. Jeshi letu la Ulinzi ni dogo, kama inavyostahili kuwa katika nchi maskini. Lakini sasa limeundwa vizuri, na limejenga vikosi vya kitaalamu vinavyotakiwa, ili lilinde mipaka yetu kutoka katika vituo muhimu. Na lina vifaa vya kutosha ingawa, kama vyombo vingine vyote, limeathirika na matatizo ya uchumi wetu katika miaka michache iliyopita. Jeshi hili, lilipoongezewa nguvu na wanamgambo waliofunzwa nalo, lilithibitisha uwezo wake katika vita vya mwaka 1978/79, na tokea wakati huo limekuwa na hekima ya kujifunza kutokana na vita hivyo. Vile vile Jeshi la Wananchi wa Tanzania limetoa mchango wake katika kupanua na kulinda uhuru wa Afrika katika nchi nyingine kwa kutoa mafunzo ndani an nje ya Tanzania. Na Jeshi la Kujenga Taifa linafanya kazi nzuri ya kutoa mafunzo ya awali ya kijeshi na ya siasa kwa wote wanaopitia humo, na katika shughuli zake za uzalishaji mali.

Jeshi letu la polisi hivi sasa linaendeshwa na Watanzania watupu; na sasa hivi ni jeshi lililoelimika zaidi kuliko lile tulilorithi. Linatoa huduma nzuri kwa

watu wa nchi hii. Bado ni jeshi dogo; ukichukua uwiano wa nchi nzima tuna polisi mmoja kwa kila watu 1,000! Lakini idadi ya makosa ya jinai yanayotolewa taarifa inaongezeka mwaka hata mwaka. Wizi wa mifugo umekuwa tatizo wakati wote katika nchi hii; lakini sasa wezi wa mifugo wakati mwingine wanashambulia mchana, na wanatumia bunduki. Mwaka 1984 matukio 1,554 ya wizi wa mifugo yalitolewa taarifa! Na kwa bahati mbaya wizi wa kutumia silaha za kila aina sasa hivi umekuwa tatizo. Polisi wanafanya juhudi kubwa kuwasaka watu wenye silaha kinyume cha sheria; kutoka mwaka 1976 silaha 897 zimekamatwa, mara nyingi kwa msaada wa raia. Lakini pamoja na kushirikiana na Kikosi cha Kuzuia Rushwa, vile vile polisi siku hizi wanalazimika kupambana na wahalifu wanaotumia ujanja mwingi, kama vile wizi wa kalamu, wizi wa fedha za umma unaofanywa na watu waliokabidhiwa madaraka, na kadhalika. Tunawahitaji wafanye vizuri zaidi katika mambo yote ya kugundua na kuzuia uhalifu; lakini badala ya kuwalaumu kwa kasoro zao, tunayo kila sababu ya kujivunia kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu sana na wakitumia vifaa ambavyo havitoshi kabisa.

Mafanikio ya polisi, pamoja na upungufu wao, ndiyo moja ya sababu ya tatizo la msongamano mkubwa wa wafungwa ambalo Magereza yetu yanajaribu kulikabili! Katika nafasi ambayo kwa taratibu zilizopo ingetosha wafungwa 19,000, wako wafungwa waliohukumiwa 29,000 na mahabusu 12,000 kwa wakati mmoja! Sehemu kubwa ya magereza haya ni ya zamani na wala hayakutunzwa vizuri, na maofisa waliopo ni kiasi cha nusu tu ya wale waliotakiwa kuwapo. Kwa hiyo huku nako tuna upungufu wa nyumba na upungufu wa maofisa!

Tunalazimika kuchukua hatua kurekebisha mambo hayo. Hatupendi kuwa na wahalifu, lakini wahalifu

ni watu, na lazima watendewe kama binadamu, ikiwa tunataka shabaha zetu za kuwarekebisha ziweze kufanikiwa. Na hiyo ndiyo juhudi inayoendelea kufanywa mpaka sasa. Inafanywa kwa utaratibu wa Magereza ya nje (na mengi ya hayo ni mfano mzuri wa kilimo bora) na kwa kutoa elimu na mafunzo kwa wahalifu wa mara ya kwanza waliohukumiwa kifungo cha zaidi ya miezi sita.

Polisi na Mahakama kwa pamoja lazima wajitahidi kuharakisha kusikilizwa kwa mashauri, maana hiyo ni kasoro kubwa katika taratibu zetu za kutoa haki. Washtakiwa wengi wanawekwa kwa kipindi cha mpaka miaka miwili kabla mashtaka yao kusikilizwa, na hali hii maana yake ni miaka miwili ya wasiwasi kwa wote wale wanaohusika, pamoja na mashahidi, na wakati mwingine muda mrefu wa kuwekwa rumande watu ambao hatimaye wataonekana kuwa hawana hatia.

Ndugu Spika. Ziko huduma nyingine nyingi sana zinazotolewa na Serikali yetu na Mashirika ya umma ambazo sikuzitaja leo. Kutokuzitaja hakuna maana kwamba huduma hizo si muhimu, wala kwamba hayakupatikana mafanikio katika maeneo hayo. Lakini hata kitabu kizima kisingetosha kueleza mambo yote tuliyoyafanya, na wala kitabu kingine kizima kisingetosha kueleza yale ambayo bado hatujayafanya!

Lakini liko eneo moja la shughuli za Tanzania ambalo ni lazima nilitaje. Kwa niaba yenu nilitamka katika Umoja wa Mataifa mwezi Desemba 1961 kwamba tulinuia kuutumia uhuru wetu kati ya mataifa kujifunza, kushirikiana na wengine, na kusaidia katika juhudi za kutafuta amani duniani na heshima ya binadamu. Nadhani tumetekeleza ahadi hiyo. Nchi hii imejipatia heshima kubwa mbele ya mataifa kwa juhudi zake na siasa yake ya kutokufungamana na upande wo wote, na kuunga mkono

Umoja wa Mataifa; imetoa mchango mzuri sana katika ukombozi wa Afrika na umoja wa Afrika, moja kwa moja na kwa kupitia Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Tunajulikana sana kwa msimamo wetu wa kupinga ukoloni na ubaguzi wa rangi, kwa maneno na kwa vitendo. Tumetoa mchango wa maana katika ushirikiano wa nchi zinazoendelea na katika jitihada za kimataifa za kuleta mfumo mpya wa uchumi duniani. Tunao Watanzania ambao ni maarufu sana dunia nzima katika mambo hayo, na Mawaziri wetu ni washiriki hodari na wenye ujuzi mwingi katika mikutano mingi muhimu na ambayo mara nyingi ni ya kitaalamu. Wanasaidiwa na watumishi wa serikali ya Tanzania walio hodari sana.

Wakati tunafanya kazi yote hii, tumekuwa tukitekeleza siasa yetu ya kutafuta urafiki na ushirikiano na mataifa yote yanayoheshimu usawa wa binadamu. Kwa sababu hiyo, na kwa sababu ya kutekeleza shabaha zetu nyingine katika nchi za nje, Tanzania ina ofisi 29 nje ya nchi hii zinazoongozwa na Balozi. Mabalozi hao wanatambuliwa katika jumla ya nchi 79 au katika Mashirika ya Kimataifa. Vile vile huwa tunamtuma Mjumbe Maalum ikiwa ni lazima kufanya hivyo; Waziri wetu wa Mambo ya Nchi za Nje ni mtu anayejishughulisha sana kwa niaba yetu katika masuala haya, na hii ndiyo sababu anakosekana mara nyingi katika Vikao vya Bunge, na ndiyo sababu ya kukosa kwake kutembelea jimbo lake la uchaguzi, au jimbo analotaka kugombea! Kwa kadiri shughuli zetu na nchi za nje zilivyoongezeka, mawaziri wengine, na hasa wale waliomo katika ofisi yangu, mara kwa mara wametumwa kufanya kazi kama hizo katika nchi za nje.

Napenda kuongeza pia kwamba tunao ushirikiano na Mabalozi 56 wanaoishi Dar es Salaam, pamoja na mabalozi wengine 25 ambao hawaishi Dar es Salaam, lakini wanazo hati za utambulisho katika Jamhuri yetu ya

Muungano. Na tunayo Mashirika ya Kimataifa 12 yenye ofisi mjini Dar es Salaam. Nachukua nafasi hii kuwashukuru wawakilishi hawa wa nchi rafiki na wa Mashirika ya Kimataifa kwa ushirikiano wao mkubwa na Serikali yetu.

Ndugu Spika. Yatakuwa makosa makubwa, na kwa kweli haitafanana na mawazo yetu wenyewe, kama nitakosa kutumia nafasi hii kuzishukuru zile nchi nyingi rafiki ambazo zimetoa na zinaendelea kutoa misaada ya maendeleo kwa Jamhuri hii ya Muungano. Mara nyingi watu wanaopenda kuzikashifu juhudi na mafanikio yetu wenyewe hutia chumvi ukubwa wa misaada tunayapokea. Lakini bado ni misaada mikubwa, na yenye manufaa makubwa. Mafanikio mengi ya kuweka msingi katika maendeleo ya uchumi na ya huduma niliyokuwa ninayaeleza yasingewezekana bila ya misaada hiyo. Misaada hiyo tumeipata kwa sababu ya juhudi zetu kubwa sisi wenyewe na kujitolea kwetu; hilo lazima lisisitizwe. Lakini bila ya misaada na mikopo yenye masharti mepesi tuliyoipokea tusingeweza kulipia vifaa vyote vilivyoagizwa kutoka nchi za nje vilivyohitajiwa kwa aina na kiasi cha kazi za maendeleo tulizozifanya. Kwa nchi chache zilizotupa misaada hiyo nimeweza kuwashukuru mimi mwenyewe, na natumaini kwamba nitaongeza kufanya hivyo kwa nchi mbili au zaidi kabla sijaaacha kiti hiki. Lakini kwa wale wote waliotusaidia, nataka kusema kwa niaba ya watu wetu wote, Asanteni sana.

Hotuba hii imekuwa ndefu mno! Niseme nini zaidi?

Tumejifunza kutembea kwa kuanza kutembea. Tumejifunza kuleta maendeleo katika nchi yetu kwa kujaribu tu kuleta maendeleo. Hatukujidai kuwa tulikuwa na ujuzi maalum wa kutuletea maendeleo; tulijua tu tunataka kwenda wapi. Kwa hiyo haikuwa ajabu kwamba wakati mwingine

mambo yetu hayakufanikiwa, au kwamba tumefanya makosa; hatukuweza wakati wote kutambua matatizo yaliyokuwa mbele yetu ambayo tulitakiwa tuyatambue. Lakini tumekuwa na ujasiri, na busara, kufanya yale yaliyoweza kufanyika kusahihisha makosa yetu, au kupambana na matatizo hayo mara tulipoyatambua. Na kwa sababu ya umoja tulioujenga na kuudumisha, pamoja na matatizo yetu yote ya miaka michache ya nyuma, tunaweza kuwa na hakika kwamba, kwa uzoefu na ujuzi wetu wa siku za nyuma, tutakuwa na uwezo kujiendeleza zaidi sisi wenyewe na nchi yetu.

Maana yako mafunzo tuliyoyapata kutokana na hayo tuliyoyafanya na tuliyofanikiwa. Sasa tunatambua wazi wazi kabisa umuhimu mkubwa wa kuongeza juhudi za kujitegemea kuwa ni njia ya kuleta maendeleo na pia ni shabaha ya maendeleo yenyewe. Tunatambua wazi wazi kabisa umuhimu wa maendeleo yaliyopangwa hatua kwa hatua; tunajua udhaifu wa maendeleo ya mori unaozuka kama cheche la moto na kuzimika kama cheche la moto, kwa jambo moja tu bila ya uhusiano na mambo mengine. Tumejifunza umuhimu wa kutunza vizuri vifaa vyetu au majengo yetu kwa wakati unaotakiwa; tumetambua kuwa ni uchumi wa kipumbavu kupuuza matengenezo ya rasilmali tuliyokwisha kuijenga. Tumejifunza kwamba mabadiliko makubwa ya muundo wa serikali lazima yataathiri uzalishaji au kuharibu huduma kwa muda. Haifai mabadiliko hayo kufanywa mara kwa mara au bila ya kufikiri sana; jambo la zuri zaidi ni kufanya mabadiliko madogo madogo wakati inapoonekana kuwa inafaa kufanya hivyo. Tumejifunza pia kwamba mkiisha kuamua kuwa jambo fulani lina umuhimu wa kwanza na ni lazima litendwe, basi ni lazima kung'ang'ania uamuzi huo bila ya kujali madai ya huduma nyingine muhimu. Maana tumetambua kwamba Kupanga ni Kuchagua.

Umuhimu wa sasa na wa miaka michache ijayo

lazima uwe ule wa kuongeza uzalishaji, na hasa uzalishaji katika kilimo. Lazima tuzalishe chakula cha kututosha mahitaji yetu kila mwaka; kuwategemea watu wengine kwa chakula kunahatarisha uhuru wetu. Na lazima tuongeze mazao tunayoyauza katika nchi za nje. Haiwezekani kufanya moja badala ya jingine; katika hali yetu yote mawili ni ya lazima kabisa. Yote haya mawili hayana budi yapewe umuhimu ule ule. Maana tunaweza tukawa na ziada ya chakula katika sehemu moja ya nchi, na watu wakafa njaa katika sehemu nyingine, kama hatukupata fedha za kigeni za kutosha kutuwezesha kukisafirisha chakula kile kutoka sehemu moja kwenda katika ile sehemu nyingine. Na wala watu hawaishi kwa mkate au kwa ugali peke yake!

Ndugu Spika. Mtu atakayeshika kiti cha Rais badala yangu, na wale watakaoingia katika Bunge hili badala ya baadhi yenu, watakuwa na matatizo makubwa sana ya kukabili. Nadhani itaonekana kutokana na haya niliyoyasema leo kwamba matatizo ya uchumi ya Tanzania hayatokani na siasa yetu ya ujamaa, bali siasa yetu ya ujamaa ndiyo iliyotupa nguvu ya kuyakabili matatizo hayo katika hali ya umoja, maelewano na matumaini. Pamoja na dalili nzuri zilozoanza kuonekana, hali ya uchumi wetu bado ni mbaya na itabaki mbaya kwa muda mrefu.

Tunadaiwa madeni makubwa sana na Mashirika ya Kimataifa, na nchi nyingine, na makampuni yaliyotukopesha vifaa; na tuna malimbikizo ya madeni ambayo yangepaswa kuwa yamelipwa, na ambayo hayawezi kulipwa upesi. Na uchumi wa dunia ambamo nasi tunajaribu kujimudu hauonyeshi dalili za kwanza kuimarika. Hata matarajio ya Shirika la Kimataifa la Fedha na ya Benki ya Dunia kwa kipindi cha miaka mitano ijayo yanaonyesha kwamba nchi maskini kabisa za dunia, ambazo ni pamoja na Tanzania, zitaendelea kuumia kwa matatizo ambayo hawana

uwezo nayo. Na baadhi ya nchi kubwa duniani zimeanza kutokuwa na moyo wa kushirikiana kimataifa; na pia zinashikilia itikadi za maguvu na maonevu. Haya yote yataendelea kuongeza matatizo ya nchi maskini duniani.

Kuhusu mambo ya siasa ya ndani namkabidhi jukumu hilo mwenzangu bila ya wasiwasi. Litakuwa jambo la lazima kwetu wakati wote kulinda na kupanua kwa vitendo uhuru na heshima tuliyowajengea raia wetu, na kurekebisha vitendo vyetu na taratibu zetu kila mazingira yanapobadilika. Gharama ya uhuru ni kuwa macho daima, ndani ya nchi na kati ya mataifa. Lazima taifa letu lipambane na tabia za rushwa na magendo zilizojitumbukiza katika kipindi hiki cha matatizo, na kuzidisha juhudi za kutambua kwamba raia wote wanao wajibu kwa nchi hii kama vile vile walivyo na haki. Na pamoja na mazingira yanayobadilika-badilika, lazima tulinde usawa, wa uchumi na wa huduma, ambao tumefanya juhudi kubwa ya kuujenga.

Tathamini hii naitoa kwa watu wetu, na pia viongozi wetu wa baadaye. Binafsi naona unyonge kidogo kuhusu yale mambo ambayo hatujayafanya bado kwa maendeleo yetu, lakini wakati huo huo najivuna sana sababu ya Nchi yetu. Mafanikio yetu ni makubwa sana. Na hasa wananchi; watu wetu sasa wanatembea kwa heshima na kujiamini; na wana haki ya kujivunia kuwa Watanzania.

Ndugu Spika na Waheshimiwa wabunge. Nawapeni wote pongezi zangu za dhati, pamoja na shukrani za moyo wangu wote kwa kazi yenu na uaminifu wenu kwa nchi yetu na watu wake wakati wa kipindi kigumu ambapo ninyi mmekuwa Wabunge wa Bunge hili. Kwa mujibu wa wajibu wenu, mmeikosoa serikali wakati mlipoona kuwa ni lazima kufanya hivyo; na wakati mwingine mmeisifia. Kwa niaba ya Wananchi wote wa Tanzania nawashukuruni kwa yote mawili.

Napenda kuongeza shukrani maalum kwa wale

waliotumika kama Mawaziri katika Serikali zote. Baadhi yao wakati mwingine wamepewa kazi ngumu mno, kulingana na nyenzo tulizoweza kuwapa. Ingawa si vizuri kumtaja mtu ye yote kwa jina, lazima nitoe shukrani maalum kwa Mawaziri wetu wa Fedha; kazi yao si kazi ya shukurani. Waziri wa Fedha hutangaza kodi, na kwa kodi hizo anapata lawama, ingawa anatamka kwa niaba ya serikali nzima; na lazima atumie sehemu kubwa ya wakati wake wa kazi kukataa maombi ambayo ni ya haki kabisa, na siku hizi hata kuwakatalia watu wenye haki ya hayo wanayoyaomba.

Uchaguzi wa Bunge utafanyika mwezi Oktoba. Baadhi ya Wabunge, miongoni mwao wakiwemo wengi waliokuwa katika Bunge hili toka uhuru wa nchi yetu na toka kuanzishwa kwa Jamhuri ya Muungano, wametangaza azima yao ya kutokugombea viti hivyo tena. Kwao hao napenda kutoa shukrani zangu maalum kwa niaba ya nchi yetu. Wote hao wamepata imani ya wananchi, na wamewatumikia vema wananchi wetu. Najua kwamba wataendelea kuwatumikia wananchi na kwamba watawasaidia wale watakaochukua nafasi zao.

Kwangu mimi mwenyewe naweza tu kusema hili moja. Tangu nilipopewa nafasi ya kuiongoza nchi yetu, kabla ya uhuru na baada ya uhuru, Wananchi wenzangu wameniheshimu na kunisaidia sana. Wangenipa nini zaidi? Kuitumikia nchi yetu na watu wake katika nafasi hii, ni heshima ya kupewa; si heshima ambayo mtu ye yote anaweza kusema kuwa anaistahili. Nilichojaribu kufanya ni kuilinda heshima hiyo, nikijua kuwa si heshima yangu, bali ni heshima ya Nchi yangu.

Shukurani ninazoweza kutoa kwa Watanzania, kwa heshima yote hiyo na msaada wote huo, ni kutoa ahadi mpya: Kwamba nitaendelea kuitumikia nchi yetu na wananchi wake kwa moyo wangu wote na uwezo wangu wote; kwamba binafsi, na katika nafasi yangu ya Mwenyekiti wa Chama

Chetu, nitamheshimu na kumsaidia Rais wa nchi yetu, tutakayemchagua wote kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu; na kwamba daima nitaendelea kusaidiana na wenzangu wote kujenga na kudumisha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Kuno kutua koleo hakuwi kwisha uhunzi;
Kupokezana koleo ni kudumisha uhunzi.
Mungu Ibariki Afrika! Mungu Ibariki Tanzania!

Asanteni sana.